Jarida La MELI

TOLEO LA 4 APRILI - JUNI 2022



USHIRIKIANO MSCL NA CCTTFA..

UK. 2



MWENYEKITI WA BODI KUENDELEZA NDOTO ZA MSCL..

UK. 4



MAOMBI YA MSCL SAFARI ZA GANA NA GODZIBA YAKUBALIWA...

UK. 9



UJENZI WA MV MWANZA WASHIKA KASI BAADA YA ZIARA YA WAZIRI MKUU

Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa na Balozi wa Korea ya Kusini nchini, Kim Sun Pyo wakiwa katika picha ya pamoja baada ya mazungumzo kati yao kwenye ukumbi wa Ofisi Ndogo ya Waziri Mkuu, Magogoni jijini Dar es salaam, Mei 14, 2022. Wengine pichani ni Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika yaMashariki, Balozi Mbarouk N. Mbarouk (kulia kwa Waziri Mkuu), Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Fred Makibete (kulia), Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Gas Entec Tanzania ambayo inatekeleza ujenzi wa meli ya MV Mwanza Hapa Kazi Tu, Dong Myung Kwak (aliyesimama nyuma katikati), Bw. Philemon Bagambilana, Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Huduma za Meli (nyuma kushoto), Kanali Samweli Mahirane, Kamishina wa Uhamiaji, Usimamizi na Udhibiti wa Mipaka nchini (nyuma kulia) na Balozi Caesar Waitara ambale ni Mkurugenzi wa idara ya Asia na Australia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki (kushoto). (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu)

Na Abdulrahman Salim

Baada ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kuagiza kukamatwa kwa pasi za kusafiria za wataalamu wa kampuni ya GAS Entec ya Korea Kusini wanaojenga meli ya MV Hapa kazi Tu jijini Mwanza tarehe 07.05.2022 na baadaye tarehe 14.05.2022 kuamuru kurudishiwa pasi hizo.

Ujenzi wa meli hiyo umeendelea kwa kasi huku ukiwa umefikia asilimia 75 hadi kufikia mwezi Juni, 2022 tofauti na ilivyokuwa wakati wa ziara ya Mhe. Kassim Majaliwa ambapo ujenzi huo ulikuwa na asilimia 65.

Katika ziara yake hiyo Mhe. Majaliwa alimuagiza Afisa Uhamiaji wa Mkoa kukamata pasi za Mkurugenzi wa GAS Entek, Bw. Dong Myung Kwak, na wasaidizi wake Bw. Kyunghan Choi na Bw. Kyuh Yun Kwak baada ya kukagua ujenzi wa meli hiyo katika bandari ya Mwanza Kusini, Wilaya ya Nyamagana, jijini Mwanza.

"Nimeingia ndani kukagua kazi ya ujenzi lakini sijaridhika nayo. Katika maelezo yao nimebaini kuwa kampuni tuliyoingia nayo mkataba ya GAS Entec imeuza share zake bila Serikali kuarifiwa. Waliouziwa, walipokuja walishangaa kuona ujenzi wa meli kwa sababu suala la ujenzi liko nje ya mauziano yao."

"Nimemwagiza Afisa Uhamiaji....

Inaendelea Ukurasa wa 8..



USHIRIKIANO MSCL NA CCTTFA KULENGA KUBORESHA USALAMA WA USAFIRI KWENYE MAZIWA

Kaimu Mhandisi Mkuu wa MSCL Mhandisi Abel Gwanafyo (wa nne toka kushoto) akitoa maelezo ya mradi wa Ukarabati wa meli ya MV Umoja kwa Katibu Mtendaji wa CCTTFA Nahodha Dieudonne Dukundane (wa pili toka kushoto) wakati wa ziara ya katibu huyo katika miradi ya MSCL mapema mwezi April,2022. (Picha na Abdulrahman Salim)

Na. Abdulrahman Salim

Shirika la Uwezeshaji wa Usafiri wa Ushoroba wa Kati (CCTTFA) limeahidi kutoa ushirikiano kwa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) katika kuboresha mawasiliano na huduma za hali ya hewa kwa usafiri wa njia ya maji ili kuwezesha uwekezaji mkubwa na kuhakikisha usafirishaji wenye usalama.

Kauli hiyo imetolewa na Katibu Mtendaji wa CCTTFA Nahodha Dieudonne Dukundane alipotembelea miradi ya ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza na ukarabati wa meli ya mizigo ya MV Umoja katika bandari ya Mwanza Kusini tarehe 6.4.2022.

"Tunajua kwamba kuna hasara nyingi zinazotokea katika maziwa ikiwemo meli kupata ajali na kuzama hali inayosababisha wawekezaji kushindwa kuwekeza katika usafiri wa njia ya maji," alimalizia.

Hata hivyo, Nahodha Dukundane ameipongeza Serikali ya Tanzania kwa uwekezaji uliofanyika katika usafiri wa reli mpya ya SGR na uboreshaji wa reli ya zamani pamoja na ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza pamoja na ukarabati wa meli ya MV Umoja.

Kuhusu fursa za kibiashara Nahodha Dukundane alisema kukamilika kwa meli ya MV Umoja kutaipatia Tanzania fursa kubwa ya kibiashara na Uganda huku akisisitiza kuwa Tanzania ina uhitaji mkubwa wa soko la Uganda.

"Soko la Uganda ni soko kubwa na ukijumlisha uwezo wa kusafirisha bidhaa katika ziwa hili ukileta zile meli za Uganda na hizi za Tanzania utaona kwa mwaka tunaweza kubeba tani karibu 300,000, lakini hizo ni kidogo ukilinganisha na tani milioni 7ambazo nchi ya Uganda huagiza kutoka nje kwa mwaka." Alisema.

Hata hivyo, Nahodha Dukundane ameishauri serikali ya Tanzania kuwa njia bora ya kuliteka soko hilo ni kwa kuongeza uwezo wa usafirishaji wa bidhaa kwa njia ya maji.

"Sisi kama Central Corridor tutaendelea kuiunga mkono serikali kupitia shirika hili la Marine Services (MSCL)kwa kuwasaidia ili wapate mabaharia wenye uzoefu," alisema.

Akiongea kwa niaba ya Afisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) Anselm Namala alisema kuwa meli hiyo ya MV Umoja ina uwezo wa kubeba tani 1,200 na inatarajiwa kukamilika mapema mwezi Februari, 2023.

"Serikali pia ima mpango wa kujenga meli mpya ya mizigo katika ziwa Victoria yenye uwezo wa kutumia reli mpya ya SGR na Meter gauge yenye uwezo wa kubeba tani 3,000 ambayo ni mara mbili na zaidi ya MV Umoja,ambayo inatarajiwa kukamilika mwaka 2025," Namala alisema.

Namala alisema kuwa uwekezaji huo pia unafanyika katika Ziwa Tanganyika ambapo ujenzi wa meli mbili mpya unatarajiwa kufanyika ili kuboresha biashara na DRC.

CCTTFA mwezi April, 2022 imepata Katibu Mtendaji mpya Wakili Flory Okandju ambae nae ameahidi kuendeleza mema yalioachwa na mtangulizi wake.

KUHESABIWA NI WAJIBU NA JUKUMU LETU.

WAJIBIKA KWA NCHI YAKO NA KWA MAENDELEO YAKO KWA KUHAKIKISHA KUWA UNAHESABIWA WAKATI WA SENSA

SENSA KWA MAENDELEO, JIANDAE KUHESABIWA

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa



MV UMOJA YAPANDISHWA CHELEZONI

Mwonekano wa Mbele ya meli ya MV Umoja ikiwa katika Chelezo (Picha na Abdulrahman Salim)

Na. Edmond Rutajama

Baada ya siku 201 kupita ambazo ni sawa na miezi sita, wiki mbili na siku sita tangu mkandarasi SM Solution kutoka Korea kukabidhiwa mradi wa Ukarabati wa meli ya MV Umoja, hatimaye meli hiyo imeingia katika hatua ya pili ya ukarabati ambayo inahusisha kuipandisha meli kwenye chelezo na kukagua upande wa chini ya mwili wa meli.

Wakati zoezi hilo likiendelea Kaimu Mhandisi Mkuu wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) ambaye pia ni meneja mradi wa ukarabati wa meli hiyo Mhandisi Abel Gwananfyo alisema kuwa amefika katika ukaguzi huo mara tu baada ya meli hiyo kupandishwa chelezoni ili kuainisha maeneo ambayo yanahitajika kufanyiwa ukarabati ili kuyapangia mikakati ya namna ya kuyarekebisha maeneo hayo.

"Leo nimepita kukagua kuona meli imekaaje katika chelezo, Je, imekaa katika mstari wake unaotakiwa, maana yake ikikaa pembezoni unaweza ukaiharibu meli, unaipindisha lakini je maeneo ambayo yamedhurika kwa kuyaangalia kwa macho, je, yapo? Ni kweli yapo, meli upande wa kulia imepinda eneo kubwa urefu kama mita 15 na zaidi, imepinda, imebonyea ikionesha kwamba kuna kitu ilikalia," Alisema.

Hata hivyo, Msimamizi Msaidizi wa Mradi huo upande wa Mkandarasi SM Solution Beda Patrick alisema kuwa kuna baadhi ya vifaa tayari vimeshawasili kwaajili ya kupachikwa katika meli hiyo baada ya zoezi la kuviondoa vifaa vya zamani kufanikiwa.

"Kuna vifaa ambavyo tayari vimeshaingia kama vile vifaa vya mawasiliano pamoja na vifaa vya umeme lakini kuna vingine ambavyo tunavitegemea kuingia hivi karibuni," Alieleza.

Ukarabati wa meli ya MV umoja unakadiriwa kumalizika mwanzoni mwa mwaka 2023 na kufanya shughuli zake za kubeba mizigo kutoka Mwanza, Tanzania kuelekea Jinja na Portbell nchini Uganda.

NAULI MPYA ZA NEW VICTORIA NA NEW BUTIAMA ZATANGAZWA

Na Fatina Msangi

Uongozi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) umewatangazia wateja na umma kwa jumla kuhusu mabadiliko ya nauli kwa meli zake zinazotoa huduma katika Ziwa Victoria kwa Meli hizo za New Victoria Hapa Kazi Tu inayofanya safari zake kati ya Mwanza na Bukoba kupitia bandari ya Kemondo pamoja na meli ya New Butiama Hapa Kazi Tu inayofanya safari zake kati ya bandari ya Mwanza Kaskazini na Nansio, Wilaya ya Ukerewe, Mkoani Mwanza.

Kwa mujibu wa MSCL wamesema kuwa ongezeko hilo ni kutokana na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji ambazo Shirika la Uwakala wa Meli imezitambua na hivyo hivyo kutoa mwongozo wa mabadiliko ya nauli hizo katika Tangazo la Serikali namba 457 la tarehe 24.06.2022.

Akizungumza katika mkutano na waandishi wa Habari, Afisa Uhusiano wa MSCL Abdulrahman Salim aliwahakikishia wateja na abiria wanaotumia huduma hizo za meli kuwa nauli hizo zimezingatia uwezo na kipato cha mwananchi mmoja mmoja na kulenga kuboresha huduma za uendeshaji.

"Viwango hivyo vipya vinatarajiwa kuanza kutumika kuanzia tarehe 04.07.2022 huku kwa meli ya New Victoria yenye madaraja matatu nauli yake itabadilika kutoka shilingi 16,000 hadi Shilingi 21,000 kwa daraja la Uchumi na kutoka Shilingi 30,000 hadi Shilingi 40,000 kwa daraja la Biashara pamoja na mabadiliko ya kutoka Shilingi 45,000 hadi Shilingi 55,000 kwa daraja la Kwanza kwa abiria wenye umri wa kuanzia miaka 12 na kuendelea." Alisema.

Hata hivyo kwa Watoto wenye umri wa kuanzia miaka 5 hadi 11 nauli hizo mpya ni Shilingi 11,000 kwa daraja la Uchumi, Shilingi 21,000 kwa daraja la Biashara na Shilingi 28,000 kwa daraja la Kwanza.

Kwa upande wa meli ya New Butiama Hapa Kazi Tu yenye madaraja mawili kumekuwa na ongezeko la shilingi 2,000 kwa kila daraja na hivyo kufanya nauli mpya kwa daraja la Uchumi kuwa shilingi 10,000 badala ya Shilingi 8,000/= na daraja la Biashara kuwa shilingi 12,000 badala ya shilingi 10,000 huku Watoto wakilipia shilingi 6,000 na shilingi 7,000 mtawalia.

Imesisitizwa kuwa bei hizi mpya ni kwa upande wa nauli za abiria tu na hazihusishi ongezeko la tozo kwa upande wa mizigo.

Mwenyekiti wa bodi kuendeleza ndoto za MSCL katika usafiri wa njia ya maji.

Na. Abdulrahman Salim

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Kampuni ya Huduma za Meli Meja Jenerali Mstaafu John Mbungo ameridhishwa na maendeleo ya utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa meli ya MV Mwanza pamoja na ukarabati wa meli ya MV Umoja na kuahidi kusimamia mipango ya serikali katika miradi hiyo.

Ameyasema hayo tarehe 01.06.20220 mara baada ya kutembelea na kukagua miradi hiyo katika eneo la bandari ya Mwanza Kusini mahala ambapo miradi hiyo inatekelezwa.

"Kwakweli I'm so impressed (nimevutiwa sana) na kazi ambazo zimefanyika na zinazoendelea kufanyika na mimi sasa naahidi kutoa chagizo kubwa katika kuhakikisha mafanikio haya yanakuwa makubwa zaidi," Alisema.

Aidha, Meja Jenerali Mst. Mbungo alielezea dhamira ya ziara yake hiyo kuwa ni pamoja na kujionea maendeleo yanayofanyika katika ujenzi wa meli za MSCL ambazo serikali imewekeza kwa kiwango kikubwa cha fedha.

"Nimefika ili kupata nini kinachofanyika na nini kinaendelea lakini pia kuhimiza wenzetu 'ma-engineer' (wahandisi) waliopo hapa kwenye 'site' (eneo la mradi) waweze kuharakisha, waweze kutumia muda wao vizuri ili kuweza kukamilisha kazi zao mapema kama ambavyo serikali inatarajia meli hizi ziende kuwahudumia wananchi mapema kadiri inavyowezekana," Alisisitiza.

Hata hivyo Mwenyekiti huyo ameahidi kuendelea kusimamia majukumu yaliyopo na kuhakikisha MSCL inafanikiwa kwa kiwango kikubwa na matarajio yaliyopo yanafikiwa huku akisifu utendaji kazi wa Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu pamoja na menejimenti yake.

"Yapo mabadiliko makubwa, mabadiliko ambayo yanatoa matumaini kwamba tunao mwelekeo mzuri, kampuni hii itakuwa moja ya kampuni kubwa sana nchini ambayo nadhani itakuwa ni sehemu mojawapo ya kujivunia sana kwamba tuna kampuni kubwa inayofanya shughuli zake za usafiri ndani ya maziwa yetu," Alisema.

Katika hatua nyingine, Mwenyekiti Mbungo alifanya kikao na watumishi wa MSCL na kuwaonya juu ya suala la kuheshimiana na kuachana na suala la majungu kazini huku akisisitiza kuwa kufanya hivyo ni kujirudisha nyuma kiutendaji na kukwamisha maendeleo ya Kampuni.

Awali Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu Bw. Philemon Bagambilana alisema kuwa ziara hiyo ya siku mbili ni ya kwanza kwa Mwenyekiti huyo wa Bodi na kuongeza kuwa katika ziara hiyo amefanikiwa kuongea na watumishi wa MSCL, menejimenti pamoja na kujionea shughuli mbalimbali zinazofanywa na MSCL ikiwemo utekelezaji wa miradi ya MV Umoja na MV Mwanza.

Meja Jenerali John Julius Mbungo aliteuliwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kuwa Mwenyekiti wa bodi ya Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) tarehe 14.03.2022 na hivyo kusubiri uteuzi wa wajumbe wa bodi hiyo kutoka kwa Waziri mwenye dhamana.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya MSCL Meja Jenerali Mst. John Mbungo (Mwenye Suti ya Kijivu) akisikiliza maelezo ya namna ya kuingoza meli kutoka kwa Nahodha Tom Faya wa Meli ya New Victoria Hapa Kazi Tu wakati Mwenyekiti huyo alipofanya ziara yake katika Meli za MSCL Jijini Mwanza.



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Uchukuzi) Dkt. Ally Possi (wa nne toka kulia) akitoa maelekezo kwa Kaimu mhandisi mkuu wa MSCL Mhandisi Abel Gwananfyo mara baada ya ziara yake ya kukagua ukarabati wa meli ya MV Umoja mapema mwezi April, 2022. (Picha na Mwandishi Wizarani)

HABARI PICHA



Watumishi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) waliposhiriki maandamano ya kimkoka katika uzinduzi wa filamu ya The Royal Tour Mkoani Mwanza. (Picha na Abdulrahman Salim)



Afisa Mkuu Daraja la pili Baharia Bravius Byarugaba (wa tatu toka kulia) akitoa maelezo kwa baadhi ya wakandarasi walioomba zabuni ya ukarabati wa meli za MT Ukerewe na MT Nyangumi mara baada ya wakandarasi hao kufika katika meli hizo kwaajili ya ukaguzi wa awali. Katika ukaguzi huo aliambatana na Mhandisi Ester Sikazwe (wa pili toka kulia) (Picha na Abdulrahman Salim)




Meneja Idara ya Masoko na Uhusiano kwa Umma Anselm Namala (wa pili toka kulia) alipofika katika studio za redio Kasibante iliyopo Manispaa ya Bukoba kwaajili ya kuendeleza shughuli za kujitangaza pamoja na kutoa ufafanuzi wa maswali mbalimbali yaliyoulizwa na wananchi juu ya huduma za meli za MSCL. Wengine ni waandishi wa Habari pamoja na Wakala wa Abiria katika kituo cha Bukoba Novatus Kisusi (kulia) (Picha na Edmond Rutajama)

Mwenyekiti wa Timu ya Ufundi na Usimamizi wa Miradi ya MSCL kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Lt. Col. Revocatus Ntare (kushoto) akitoa ufafanuzi kwa Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu MSCL Philemon Bagambilana (kulia) katika eneo la injini ya meli ya MT Sangara. (Picha na Abdul-rahman Salim)



MIRADI YA UKARABATI YA MV UMOJA NA MV SANGARA YAENDELEA KUPOKEA VIFAA



Baadhi ya vifaa kwaajili ya kubadilisha mifumo ya uendeshaji wa meli ya MV Umoja viliposhushwa kutoka kwenye Kontena lililotoka bandari ya Dar es Salaam vikiwa katika makasha ya mbao mbele ya ofisi ya Mkandarasi SM Solution katika eneo la bandari ya Mwanza Kaskazini, Jijini Mwanza (Picha na Mwandishi maalum)

Na. Fatina Msangi

Miradi ya Ukarabati inayohusisha meli inayobeba mizigo ya MV Umoja inayofanya shughuli zake Ziwa Victoria pamoja na meli inayobeba mafuta ya MT. Sangara inayofanya shughuli zake Ziwa Tanganyika imeendelea kupokea makontena yenye shehena za vifaa mbalimbali vinavyohusisha kubadili mifumo mbalimbali ya meli hizo kutoka mfumo wa zamani wa analogia na kuwa katika mfumo wa kidigiti.

Makontena hayo yaliyotoka bandari ya Dar es Salaam yamepokelewa katika siku tofauti katika wiki ya kuanzia tarehe 6 hadi 10 ya mwezi Juni, 2022 yakiwa na vifaa tofauti huku Kontena lililowasili Bandari ya Kigoma likiwa na vifaa vya mfumo wa umeme huku kontena lililowasili katika Bandari ya Mwanza Kusini likiwa limesheheni vifaa vya kisasa vya mfumo wa mawasiliano kwaajili ya kuwekwa katika chumba cha kuongozea meli.

Mradi wa ukarabati wa meli ya MV Umoja unatekelezwa na kampuni ya SM Solution kutoka Korea Kusini na kutarajiwa kukamilika baada ya miezi 15 hadi kukamilika kwake itagharimu shilingi bilioni 19.8 inatarajiwa kuwa na uwezo wa kubeba makontena 21 badala ya uwezo wa sasa wa kubeba makontena 19. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwaka 2023.

Mradi wa ukarabati wa Meli ya MT. Sangara unatekelezwa na Kampuni ya KTMI kutoka Korea Kusini na Kutarajiwa kukamilika baada ya miezi 12 na hadi kukamilika kwake itagharimu shilingi bilioni 8 na kubebe lita 410,000 ambayo ni sawa na tani 350. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2022.

Meneja Mradi wa ujenzi wa MV Mwanza Mhandisi Vitus Mapunda akitoa taarifa ya utekelezaji wa ujenzi wa meli ya MV Mwanza kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Huduma za Meli Meja Jenerali Mstaafu John Mbungo baada ya kuwasili kwa ajili ya kukagua mradi huo.

NAULI MPYA ZATANGAZWA...UK. 5



Watumishi wa Kamouni ya Huduma za Meli wakiongozwa na Wakala wa Abiria kituo cha Kemondo Aboubakar Kaponta (katikati) walipofika katika studio za Redio Lumuli iliyopo Manispaa hya Bukoba ili kufafanua juu ya kupanda kwa nauli za abiria katika meli za MSCL zinazotoa huduma zake katika Ziwa Victoria, Kulia ni Afisa habari MSCL Fatina Msangi na Afisa Utekelezaji Marwa Marwa. (Picha na Mwandishi Maalum)

Ujenzi wa MV Mwanza washika kasi baada ya ziara ya waziri mkuu..



Waziri Mkuu, Mhe.Kassim Majaliwa akiondoka eneo la mradi wa ujenzi wa meli mpya ya MV Mwanza tarehe 07.05.2022. (Picha na Ofisi ya Waziri Mkuu)

Inatoka Ukurasa wa kwanza

....wa Mkoa akamate pasi zao mara moja na ahakikishe hakuna mtu anatoka nje ya mkoa huu hadi hii kazi ikamilike. Nimeambiwa wako saba, lakini hapa wako watatu. Watafuteni hao wengine wako wapi."

Waziri Mkuu alisisitiza kuwa Serikali ilishalipa asilimia 80 ya gharama za ujenzi wa meli hiyo lakini kazi iliyofanyika kwa mujibu wa mkataba ni asilimia 65 tu. Amesema taarifa alizonazo zinaonesha kuwa wafanyakazi walikuwa 118 lakini sasa wamebakia 22 tu.

Aidha alisema kuwa maamuzi hayo yanaridhaa ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan. "Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuridhia hatua hii."

"Hawa watu wasiondoke hadi kazi ikamilike na kama wataondoka basi atakayewadhamini ni Balozi wao. Serikali tutaendelea kuwasiliana na Balozi wa Korea Kusini na tunaamini kazi hii itakamilika. Wizara husika simamieni na kuhakikisha kazi inakamilika kwa mujibu wa mkataba."

Waziri Mkuu amesema hakuna mradi wa kimkakati ambao utakwama. "Mheshimiwa Rais ameagiza tusimamie hii miradi, nasi ndiyo maana tuko tuko barabarani kila siku Ninawaomba Watanzania muamini kuwa Serikali yenu iko imara. Na pia niwahakikishie viongozi wa Chama cha Mapinduzi mliopo hapa kwamba Ilani yetu itatekelezwa kwa zaidi ya asilimia 90," amesema.

Katika kuhakikisha mradi huo unafanikiwa Waziri Mkuu alikutana na Balozi wa Korea Kusini nchini, Kim Sun Pyo kwenye ukumbi wa Ofisi Ndogo ya Waziri Mkuu, Magogoni jijini Dar es salaam, tarehe 14.05.2022 pamoja na uongozi wa Kampuni ya Gas Entec Tanzania na kuitaka Kampuni hiyo kuzingatia makubaliano yote yaliyomo kwenye mkataba wa ujenzi wa meli hiyo kabla ya kuruhusu kurudishiwa kwa pasi za kusafiria za wataalamu hao.

Katika Kikao hicho ambacho kilihudhuriwa Mkurugenzi wa Kampuni ya Gas Entec Tanzania Bw. Kwak ambaye alikiri mapungufu katika utekelezaji wa mradi huo na aliahidi kuwa kampuni yake itaongeza kasi ya ujenzi ili ukamilike kwa wakati na meli hiyo iweze kuwahudumia wananchi kama ilivyokusudiwa.

Kikao hicho pia kilihudhuriwa na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, Mbarouk Mbarouk na Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Fred Mwakibete. Wengine ni Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Huduma za Meli, Philemon Bagambilana na Kanali Samwel Mahirane ambaye ni Kamishina wa Uhamiaji, Usimamizi na Udhibiti wa Mipaka nchini.

Gharama za ujenzi wa meli hiyo ni dola za Marekani milioni 39 sawa na Sh Bilioni 97 na itafanya safari zake katika nchi zote ambazo ziko ukanda wa ziwa Viktoria na ikikamilika itakuwa na uwezo wa kubeba abiria 1200 na tani 400 za mizigo, magari madogo 20 na magari makubwa 3.

Septemba 3, Mwaka 2018 serikali iliingia mkataba wa ujenzi wa meli ya MV Mwanza Hapa Kazi tu na kampuni ya GAS Entec ya Korea Kusini ikiwa ni mbadala wa meli ya MV Bukoba iliyozama mwaka 1996 na mradi huo unasimamiwa na Kampuni ya Huduma ya Meli nchini (MSCL).

Tutembelee kwenye mitandao yetu ya kijamii

Kampuni ya Huduma za Meli

mscltz MSCLtz Meli TV

Maombi ya MSCL safari za Gana na Godziba yakubaliwa na TASAC

Na Abdulrahman Salim

Shirika la Uwakala wa Meli (TASAC) wameiruhusu Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) kuanzisha safari za kwenda visiwa vya Gana na Godziba kutokea mwalo wa Kirumba Jijini Mwanza kwa kutumia meli zake za MV Clarias na ML Wimbi.

Ruhusa hiyo imetolewa kupitia amri ya nauli za abiria kwa usafiri majini iliyotoka katika Tangazo la Serikali namba 458 la terehe 24.06.2022 na kuitaka MSCL kuzingatia viwango vya usalama kama vilivyotolewa katika Sheria ya Usafiri Majini na Kanuni zake.

Aidha, mchakato huu wa kupatikana kwa ruhusa hii ulianzia baada ya Uongozi wa MSCL kufanya ziara ya utafiti wa masoko katika visiwa vya Gan ana Godziba mapema mwezi Januari mwaka 2022 na kupata maoni kutoka kwa wananchi wanaoishi katika visiwa hivyo na hatimae kulifikisha suala hilo TASAC ili kuomba ridhaa ya kuendelea na huduma katika visiwa hivyo.

Akizungumza wakati wa Ufunguzi wa mkutano wa wadau Mwenyekiti wa Kikao hicho Mkurugenzi wa Udhibiti Uchumi kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu TASAC Nason Sigara alisema kuwa wito wa kikao hicho ni kupokea kupokea maoni juu ya kuanza kwa safari za meli za MSCL katika visiwa vya Gana na Godziba na kuwa si lazima kila swali litakaloulizwa lipatiwe majibu.

Akiongea kwa niaba ya wananchi wa Kisiwa cha Gana Mwenyekiti wa Kijiji cha Kamasi kinachojumuisha Kisiwa hicho Frank Matondane maarufu kama Deco alikubaliana na nauli zilizopendekezwa na MSCL kwenye wasilisho lao katika kikao hicho kabla ya TASAC kuanza kupokea maoni ya wadau.

"Nipo hapa kwa niaba ya watu wa Gana na pia nawakilisha Serikali ya Kijiji cha Kamasi ambayo ina visiwa 12, Mheshimiwa Mwenyekiti lazima tuseme ukweli kwamba kwa sasa mafuta yamepanda bei, lazima tukubaliane tu kwamba nauli zimepanda, hiyo shilingi 9,000/= kwenda Gana kutoka Mwanza ni sahihi kabisa kwasababu, yawezekana leo tukalazimisha iwe shilingi 8,000/= lakini baada ya miezi miwili ikaja lugha nyingine kwamba mafuta yameongezeka bei na nauli tunapandisha," alisema.

Kwa upande wake Afisa Utekelezaji wa MSCL Antony Stephen wakati akiwasilisha mada ya kuomba ridhaa ya kuanzisha kwa safari ya visiwa vya Gana na Godziba mbele ya wadau hao alisema kuwa bei hizo pendekezwa za abiria na mizigo zimetokana na maoni yaliyokusanywa na Kampuni kutoka kwa wasafirishaji wa njia hizo pamoja na gharama za uendeshaji wa meli hizo.

"Athari zitakazotokea endapo nauli zilizopendekezwa zisipokubaliwa ni meli hizo kushindwa kujiendesha kwa faida, pia tutashindwa kumudu gharama za ununuzi wa vipuri, tutashindwa kununua mafuta, vilainishi vya mitambo (Injini), tutaushindwa kulipa mishahara ya watumishi, tutashindwa kutoa gawio Serikalini, tutashindwa kulipa mirahaba kwa taasisi mbalimbali ikiwemo TASAC," Alifafanua.

Aidha, katika Tangazo la Serikali Namba 458, TASAC wamepitisha nauli ya Shilingi 16,500 kutoka Mwalo wa Kirumba kwenda Godziba na nauli ya Shilingi 10,500 kutoka Mwalo wa Kirumba kwenda Gan ana nauli ya Shilingi 6,000 kutoka Gana kwenda Godziba.

Mafanikio haya yamesababishwa na juhudi za uongozi wa MSCL baada ya kutuma timu yake iliyoongozwa na Meneja Masoko na Uhusiano kwa Umma Anselm Namala kwa kufika katika visiwa hivyo tarehe 4 hadi 8 Januari, 2022, kukutana na wananchi na wafanyabiashara na kisha kufanyika kikacho cha wadau cha TASAC katika ukumbi wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza tarehe 08.04.2022 na hatimae tarehe 24.06.2022 tangazo la kukubaliwa kuchapishwa.



Mwenyekiti wa kikao cha kupokea maoni ya wadau kuhusu bei za nauli na tozo za safari za meli za MV Clarias na ML Wimbi, Mkurugenzi wa Udhibiti Uchumi TASAC Nason Sigara (wa tano toka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na wadau hao wakiwemo wakazi wa visiwa vya Gan ana Godziba pamoja na watumishi wa MSCL waliongozwa na Afisa Masoko Mkuu Eugenia Punjila (wa nne toka kulia) (Picha na Abdulrahman Salim)

Inatoka ukurasa wa 3



Timu ya Mpira wa miguu ya Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) wakiwa tayari kwaajili ya mechi ya kirafiki na timu ya Mamlaka ya Bandari (TPA) tawi la Mwanza (Picha na Mwandishi Maalum)



Watumishi wa Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) walioshiriki katika maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani wakiwa katika picha ya pamoja. (Picha na Edmond Rutajama)

SHUKRANI ZA KIPEKEE KWA KUFANIKISHA JARIDA HILI

BODI YA WAHARIRI

MWENYEKITI - PHILEMON BAGAMBILANA
MHARIRI - ABDULRAHMAN SALIM

WAJUMBE

ANSELM NAMALA
BARAKA BIGAMBO
MHANDISI ABEL GWANAFYO
NAHODHA BEMBELE NG'WITA

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

JARIDA HILI IMEANDALIWA NA KUTOLEWA NA KAMPUNI YA HUDUMA ZA MELI

RC Andengenye aahidi kufanya kazi na MSCL bega kwa bega

Na Abdulrahman Salim

Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Kamishna Jenerali Mst. Thobias Andengenye ameahidi kutoa ushirikiano wa karibu katika kusimamia utekelezaji wa miradi ya Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) inayofanyika katika bandari ya Kigoma, mkoani humo.

Mh. Andengenye amesema kuwa ushiriki wake katika kusimamia na miradi hiyo hahitaji kutengewa bajeti yoyote na MSCL na badala yake anahitaji kuarifiwa juu ya kinachoendelea na kutoa msaada pale inapobidi ili kusaidia kukamilisha utekelezaji wa miradi hiyo.

"Sisi na Marine Services Company Limited hatuhitaji bajeti kwaajili ya kwenda kufanya kazi, hata mafuta yakiisha hapa tunatembea kwa miguu, Mkitaka kunialika pale hamna ulazima wa kusema aah mimi sina bajeti ya kumuita Mkuu wa Mkoa aje aangalie, sihitaji bajeti yoyote nahitaji tu kuarifiwa kwamba bwana njoo kidogo utembee uje uone wala sihitaji chai wala zaidi ya kusaini kitabu cha wageni," Alisema.

Aidha, aliwasihi viongozi wa MSCL kuhakikisha hawamsahau katika vichwa vyao na kumshirikisha kwa kila jambo linalotokea kwenye miradi na kusisitiza kuwa yupo pamoja kwenye safari ya kuhakikisha miradi hiyo inafanikiwa.



Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Kamishna Jenerali Mst. Thobias Andengenye (Kulia) akiongea na Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa MSCL Philemon Bagambilana (kushoto) pamoja na timu ya Ufundi na Usimamizi wa Miradi ya MSCL (hawapo pichani) muda mfupi baada ya kupokea taarifa ya miradi inayotekelezwa na MSCL Mkoani humo. (Picha na Abdulrahman Salim)



Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Kamishna Jenerali Mst. Thobias Andengenye akimsikiliza kwa makini Mwenyekiti wa Timu ya Ufundi na Usimamizi wa Miradi kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Lt. Col. Revocatus Ntare, baada ya timu hiyo kufika katika ofisi hiyo ili kujitambulisha shughuli zao katika miradi inayosimamiwa na MSCL (Picha na Abdulrahman Salim)

Mhe. Andengenye aliyasema hayo alipotembelewa na Uongozi wa MSCL ukiongozwa na Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu Philemon Bagambilana pamoja na Mwenyekiti wa Kamati ya Ufundi na Usimamizi wa miradi ya MSCL kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi Luteni Kanali Revocatus Ntare wakati walipofika katika ofisi hiyo kwa nia ya kumjulisha uwepo wa kamati hiyo pamoja na kumpa taarifa fupi ya mradi unaoendelea pamoja na miradi inayotarajiwa kufanyika mkoani humo.

Wakati akitoa taarifa fupi ya mradi wa meli ya MT. Sanagara Bagambilana alisema kuwa mradi huo tayari umeshapokea awamu tatu za vifaa vya ukarabati wa meli hiyo na kutaraji kupokea awamu ya nne ya vifaa ifikapo katikati ya mwezi Julai, 2022 wakati mradi ukitarajiwa kukamilika mwezi Novemba, 2022.

Meli ya MT. Sangara inakarabatiwa na Mkandarasi KTMI Co. Ltd kutoka nchini Korea kwa thamani ya zaidi shilingi bilioni 8 na kutarajiwa kukamilika mwezi Novemba mwaka

SENSA KWA MAENDELEO, JIANDAE KUHESABIWA

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa

KAMPUNI YA HUDUMA ZA MELI (MSCL)
BANDARI YA MWANZA KASKAZINI, JENGO LA TPA, SAKAFU YA PILI
S. L. P. 2385, MWANZA, Hotline: +255 739 606 600
Barua Pepe: info@mscl.co.tz Tovuti: www.mscl.co.tz
Kampuni ya Huduma za Meli MSCLtz mscltz Meli TV
JARIDA HILI IMEANDALIWA NA KUTOLEWA NA KAMPUNI YA HUDUMA ZA MELI NCHINI